## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
## HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI

SHULE YA SEKONDARI MSHIKAMANO,
S.L.P. 50,
MBARALI – MBEYA.

TAREHE ............................

KUMB,NA.....................
JINA LA MWANAFUNZI ..................................................
S.L.P. ...................
.....................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MSHIKAMANO WILAYA YA MBARALI MKOA WA MBEYA MWAKA ..........................**

1. Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha ............ Katika shule hii mwaka .................... shule ya sekondari mshikamano ipo umbali wa km 02 kasikazini / mashariki/magharibi/kusini mwa mji mkuu wa mkoa/wilaya ya mbarali – Mbeya
2. Mhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe .............................. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe .................. (ndani ya siku saba ukichelewa zaidi ya hapo hutapokelewa)
3. Bidii ya kujituma katika masomo, utii, uaminifu, nidhamu bora, maarifa na juhudi kwa pamoja/ ujumla vitakuwezesha kuwa na mafanikio mazuri kitaaluma na kujijengea tabia na mwenendo mzuri endelevu

1.0. MAMBO MHIMU YA KUZINGATIA
SARE YA SHULE

1.1. WAVULANA

(i) Suruali mbili (02) moja ya rangi ya kijivu na nyingine ya rangi ya zambarau. Suruali ziwe zina malinda mawili (2) mbele. Tafadhali
(ii) Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi
(iii) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba
(iv) Soksi rangi nyeupe zisizo na pambo au mapambo yeyote yale
(v) Mkanda wa kiunoni wa kuvalia suruali uwe wa ngozi na rangi nyeusi
(vi) Sweta rangi ya kijani. Tafadhari liwe jipya
(vii) Bukta ya rangi ya blue na tisheti ya rangi ya zambarau kwa ajili ya michezo

2.0. WASICHANA

(i) Sketi mbili (2) moja ya rangi ya kijivu na nyingine rangi ya zambarau. Tafadhari sketi zote mshono wake ziwe wa (LINDA BOKS) na ziwe ndefu sana
(ii) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mifupi
(iii) Viatu vya ngozi nyeusi vya kufunga na kamba
(iv) Soksi rangi nyeupe zisizo na pambo au mapambo yoyote yale
(v) Sweta la rangi ya kijani. Tafadhari liwe jipya
(vi) Hijabu rangi nyeupe
(vii) Bukta ya rangi ya Blue na Tisheti ya rangi ya zambarau kwa ajili ya michezo

***NB" Mwanafunzi ambaye sare yake haitakidhi matakwa ya shule hatavumiliwa"***

2.1. Daftari kubwa 9 na mkebe mmoja (1) kwa kila mwanafunzi
2.2 Chakula cha mchana, nauli ya kuja shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu endapo mwanao ataugua akiwa shuleni.

0. **SHERIA NA KANUNI MHIMU ZA SHULENI**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 aidha. Inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

(a) Heshima kwa viongozi wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
(c) Kushiriki kwa makini vipindi vyote vya darasani
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
(i) Kutunza mali za umma

3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule
(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(g) Kudharau bendera ya Taifa
(h) Kuwa mjamzito / kupata mimba
(i) Kuoa au kuolewa
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma. Kuchochochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi
(m) Kuwa na simu ya mkononi

**Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

(a) Medical Examination form, ambayo itajzwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule

Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatelekeza kikamilifu

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....................................

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MSHIKAMANO
S.L.P. 50
IGURU...

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**SHULE YA SEKONDARI MSHIKAMANO**
**FOMU YA KIAPO CHA UTII**

Mimi ________________________________________________ niliyeteuliwa kujiunga na masomo katika shule ya Sekondari mshikamano. Naapa kwamba nitakuwa mwaminifu, mwadilifu na mtii kwa walimu, wafanyakazi wasiokuwa walimu. na wanafunzi wenzangu

Kwa nafasi hii adimu niliyoipata naahidi kwamba nitasoma kwa bidii na kwa juhudi zangu zote ilinije kuwa raia mwema wan chi yangu ya Tanzania, na ninaahidi kuwa sitakuwa chanzo cha migogoro yoyote niwapo shuleni na nje ya mipaka ya shule.

Yote haya nitayatekeleza kwa kutovunja sheria, taratibu na kanuni zote zilizowekwa na shule, nikienda kinyume basi sheria kali ichukuliwe ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

*EEE MWENYEZI MUNGU NISAIDIE*

Sahihi ya muapaji ______________________________ Tarehe________________

Sahihi na mhuri wa msimamizi wa kiapo ........................................... tarehe ..........

***Sehemu hii ijazwe na mzazi au mlezi wa mwanafunzi kukiri/ kukubali kwa mzazi/ mlezi kugharamia mahitaji ya mwanafunzi***

Mimi ________________________________________ mzazi / mlezi wa ________________________________________ Ninakubali kumgharamia mwanafunzi huyu mahitaji yake yote. Nakiri nimesoma taarifa hii iliyotoka kwa mkuu wa shule ya sekondari Mshikamano na nimeelewa kikamilifu

Naahidi kwamba nitatimiza mahitaji yote yanayotakiwa katika kusomesha mwanafunzi huyu hadi mwisho. Nikishindwa kuwajibika nichukuliwe hatua zinazofaa ikiwa ni pamoja na kushitakiwa mahakamani..

**Sahihi ya Mzazi/ Mlezi** ________________________________

**Tarehe**..........................................................................

FOMU D

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING

Mshikamano Sekondari School.
P.O.BOX 50,
IGURUSI.

Date ..........................

Ref: No. MSS/JI/1/02 ..................

The Medical Officer.

..................................

..................................

..................................

Please examine ........................................................................................ as for her/his fitness for pursuing further education in this school.

1. Hemoglobin ....................................................................................................
2. P.V. Bleeding ....................................................................................................
3. (a) Weight ....................................................................................................
4. Blood pressure ....................................................................................................
5. Urine for sugar and pregnancy ....................................................................................
6. Stool ....................................................................................................
7. Asthma ....................................................................................................
8. Skin Disease ....................................................................................................
9. Lepresy ....................................................................................................
10. Eplopsy ....................................................................................................
11. Pulmonary tuberculosis ....................................................................................
12. Mental problems ....................................................................................................

**COMMENTS OF THE MEDICAL OFFICER**

....................................................................................................................................
....................................................................................................................................
....................................................................................................................................
....................................................................................................................................

# MHUTASARI WA MKUTANO WA WAZAZI SHULE YA. MSHIKAMANO SECONDARY SCHOOL KUHUSU CHAKULA SHULENI TAREHE 18/07/2016

MAHUDHURIO.

WAZAZI WALIKUWA 260.

MAKUBALIANO WALIKUBALIANA WACHAGUE KAMATI.

1. MWENYEKITI - FEDRICK MWAKABANGA.
2. KATIBU - BENJAMINI MWAKAJWANGA.
3. KATIBU MSAIDIZI - JOEL AMBONISYE.
4. MAKAMU MWENYEKITI - PACK LUPAKISYE.
5. MHASIBU – VUMILIA KOMAKULINGA.

WASIMAMIZI WA KIKAO HICHO NI:

- MTENDAJI – JORDANI MAPUNDA.
- AFISA USHIRIKA (MDAU ELIMU KATA).
- BIBI MAENDELEO. WINNI.
- MKUU WA SHULE – RASHIDI.
- MRATIBU – SAVINITU.

WAZAZI WALIKUBALIANA MCHANGO KAMA IFUATAVYO KWA KILA MTOTO;

1. MAHINDI LITA KUMI YA KUKOBOLEWA ILIYOJAA.
2. MAHARAGE (Walikubaliana kuchangia fedha Tsh. 7000/=).
3. MAFUTA LITA MOJA.Tshs 3500/=.
4. CHUMVI PAKITI MOJA Tsh. 500/=
5. PESA KWA AJILI YA MPISHI NA KUNI Tsh .4000/=.

Makubaliano hayo ni ndani ya miezi sita ambayo kwa mwaka ni mala mbili yake. Wazazi walisisitiza kuwa asiyechanga afikishwe mahakamani na wote kwa pamoja wakakubaliana pia walikubaliana mwisho wa mchango itakuwa tarehe **30/08/2016**. Na utekelezaji wa watoto kula chakula shuleni uanze na mwisho kikao kilihairishwa na Mwenyekiti **FEDRICK MWAKABANGA** kuwashukuru viongozi wa kata pamoja na wazazi wote waliohudhuria kikao hicho shuleni na kuwaambia wazazi watoe kwa wakati ili kuondoa usumbufu wakufikishwa mahakamani. Kikao kilihaurishwa saa 7:4 Mchana. Pia tunaambatanisha na mahudhurio ya kikao hicho.

MWENYEKITI ________ KATIBU ________

KAMATI YA WAZAZI YA KUBORESHA TAALUMA MSHIKAMANO SEKONDARI